TANZANIA DAIMA UK 8

Wafanyabiashara wa nyama waonywa

NA JANETH JOVIN

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka, Wafanyabiashara wanaouza nyama nchini kutopandisha bei ya kitoweo hicho hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Sikukuu ya Idd el fitr.

Aidha Ulega amemtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri ndani ya siku saba kuhakikisha wanawapeleka wafanyabiashara wanaofanya biashara katika machinjio ya vingunguti kwenye eneo lao jipya walilotengewa na Manispaa hiyo.

Waziri Ulega aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akikagua ujenzi wa mradi wa machinjio ya kisasa katika eneo la Vingunguti lilipo katika Manispaa hiyo.

Ulega alisema, wafanyabiashara wa nyama wanapaswa kuuza kwa bei ya kawaida kulingana na hali ilivyo ili kuhakikisha watu wote wanapata kitoweo hicho.

Alisema imekuwa ni kawaida kwa wafanyabiashara ya nyama kupandisha bei kipindi cha Sikukuu kinapofika wakati wakijua kuwa kufanya hivyo ni kuwakwamisha wananchi kupata nyama kulingana na bei kuwa juu.

"Serikali ya awamu ya tano inatengeneza uchumi endelevu hivyo katika kuhakikisha hili wafanyabiashara wa nyama wanatakiwa kuchangamkia fursa ya Sikukuu ya Idd katika kuuza nyama kwa bei ya kawaida na sio ya kuwaumiza wananchi," alisema

Ulega alisema, mradi wa machinjio ya kisasa ya vingunguti hadi sasa umefikia asilimia 85 ya ukamilikaji wake na tayari mashine zipo katika kutendelea kufanya kazi.

Alisema mradi huo unaogharimu Sh.Bilioni 12.4 unalengo la kuhakikisha wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam, mikoa mingine na nchi za nje kupata nyama itakayokuwa bora na yenye kuandaliwa vizuri.

"Wizara yangu ndio inashughulikia masuala ya mifugo natoa pongezi kwa Serikali kwa hatua hii ya kufikisha jengo hili katika kiwango cha juu kwani kiwanda pekee kinachotusaidia kwa sasa kipo Mwanza hivyo kupitia kiwanda hiki naamini tutaongeza nguvu katika uuzaji wa nyama," alisema na kuongeza

"Ukamilikaji wa machinjio haya yatatoa fursa kwa Serikali kuuza nyama hadi nje ya nchi na tunaamini wanunuzi wataridhika zaidi kutokana na uwekezaji tunaouweka katika mradi huu," alisema na kuongeza

"Bado tunafursa nyingi katika kuhakikisha nyama inapatikana kwa wingi na tutaacha ununuaji wa nje ya nchi pindi mradi huu utakapokamilika na tutahakikisha sisi ndio tunawapelekea watu wa nchi nyingine."

Alisema eneo hilo litachinja ng'ombe takribani 1500 na mbuzi 1000 kwa siku moja pindi itakapokamilika hivyo upandishaji holela wa bei ya nyama kwa vipindi vya Sikukuu hautakuwepo tena kutokana na nyama kupatikana kwa urahisi zaidi.

Naye Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Imani Sichalwe alisema, kupitia mradi huo wafugaji watapata masoko makubwa na kutoingiliwa na madalali ambao kwa asilimia kikubwa walikuwa wanawalalia.

Alisema ni wakati wa wafugaji kujipanga na kuanza kufuga kwa kisasa kwa kuongeza ubora na thamani ya mifugo yao.



mko iana. viko. (Na

7/-

esa hivyo a huduma uwa watu uwezesha liongeza. alisema, ababisha ao hasa lha kwa

aendelea kuongeza uchochea ara. igo Pesa biashara kote na naosaidia siku.

Scanned with CamScanner

Omary Mgumba.
(Na Mpigapicha Wetu)

MAJIRA UK 11

Wafanyabiashara watakiwa kutopandisha bei ya nyama Idd

Na Penina Malundo

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wafanyabiashara wanaouza nyama nchini kutopandisha bei wakati wa Sikukuu Idd el fitr ili wananchi wapate kitoweo hicho kwa bei nafuu.

Pia amemtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala Jumanne Shauri ndani ya siku saba kuhakikisha wanawapeleka wafanyabiashara wanaofanya biashara katika machinjio ya vingunguti kujionea eneo jipya lililotengewa na Manispaa ya Ilala.

Naibu Waziri Ulega alitoa agizo hilo wakati akikagua ujenzi wa miradi wa machinjio ya kisasa katika eneo la vingunguti uliopo Manispaa ya Ilala.

Alisema wafanyabiashara wa nyama wanapaswa kuuza nyama kwa bei ya kawaida kulingana na hali ilivyo ili kuhakikisha watu wote wanapata kitoweo hicho.

Alisema imekuwa ni kawaida kwa wafanyabiashara ya nyama kupandisha bei kipindi cha sikukuu kinapofika hawajui kufanya hivyo ni kukwamisha wananchi kutopata nyama kwa kuuzwa bei ya juu.

Ulega alisema wafanyabiashara hao wakatumia fursa ya sikukuu kwa kuuza nyama kwa uhakika huku kutoongeza bei ya bidhaa hiyo.

"Serikali ya awamu ya tano inatengeneza uchumi endelevu, hivyo wafanyabiashara wa nyama wanatakiwa kuchangamkia fursa ya sikukuu ya Idd katika kuuza nyama kwa bei ya kawaida na sio ya kuwaumiza wananchi," alisema

Aidha alisema mradi wa machinjio ya kisasa ya vingunguti hadi sasa yamefikia asilimia 85 ya ukamilikaji wake na tayari mashine zipo katika kutendelea kufanya kazi.

Alisema mradi huo unaogharimu kiasi cha sh. billioni 12.4 ambao una lengo la kuhakikisha wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam, mikoa mingine na nchi za nje kupata nyama itakayokuwa bora na yenye kuhandaliwa vizuri kutokana na jengo hilo.

"Wizara yangu ndio inashughulikia masuala ya mifugo natoa pongezi kwa Serikali kwa hatua hii ya kufikisha jengo hili katika kiwango cha juu kwani kiwanda pekee kinachotusaidia kwa sasa kipo Mwanza hivyo kupitia kiwanda hiki naamini tutaongeza nguvu katika uuzaji wa nyama," alisema na kuongeza

"Ukamilikaji wa machinjio haya kutatoa fursa kwa Serikali kuuza nyama hadi nje ya nchi na tunaamini wanunuzi wataridhika zaidi kutokana na uwekezaji tunaouweka katika mradi huu," alisema Ulega

Alisema uwekezaji wa mradi huu utailipa Serikali katika hatua zote ikiwemo kiuchumi na kijamii pindi shughuli za mnada zitakapoanza kufanyika katika jengo hilo.

Ulega alisema Tanzania bado ina fursa nyingi katika mifugo na Serikali tayari ina mikakati mizuri ya kuhakikisha sekta hii inazidi kukua siku hadi siku na kutoagiza nyama nje ya nchi.

"Bado tuna fursa nyingi kuhakikisha nyama inapatikana kwa wingi na tutaacha ununuaji wa nje ya nchi pindi mradi huu utakapokamilika na tutahakikisha sisi ndio tunawapelekea watu wa nchi nyingine" alisema

Alisema eneo hilo litachinja ng'ombe takribani 1,500 na mbuzi 1000 kwa siku moja pindi itakapokamilika hivyo upandishaji holela wa bei ya nyama kwa vipindi vya Sikukuu hautakuwepo tena kutokana na nyama kupatikana kwa urahisi zaidi.

Scanned with CamScanner

Kwa Ufupi

Upelelezi kesi vigogo wa Halotel haujakamilika

Dar es Salaam. Upelelezi wa kesi inayowakabili wafanyakazi sita wa kampuni ya Halotel akiwamo mkurungenzi mtendaji, Son Nguyen (46) bado haujakamilika.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 10 likiwamo la kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara ya Sh78 bilioni.

Mbele ya hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Jana, wakili wa Serikali, Candid Nasua alisema upelelezi bado haujakamilika hivyo, hakimu mkazi mkuu, Thomas Simba kuliahirisha shauri hilo.

Mbali ya Nguyen wengine ni mameneja wa kampuni hiyo, Nguyen Minh (40), Vu Tiep, Ha Than (39) ambaye mtaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), mkurugenzi wa fedha, Nguyen Cong (35) na kampuni ya Viattel ambayo imesajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Kati ya mashtaka 10 yanayowakabili yamo ya kutakatisha fedha na kuisababishia hasara Serikali.

(Pamela Chilongola)

MSD kusitisha huduma kwa siku 21

Dar es Salaam. Bohari ya Dawa (MSD) imetangaza kusitisha huduma kwa siku 21 kuanzia Juni 10 mpaka Juni 30 ili kujipa nafasi ya kuhakiki mali ilizonazo.

Kwa uamuzi huo, maghala ya bohari hilo yatafungwa hivyo imewataka wateja wake hususan vituo vyote vya huduma za afya nchini kupeleka maombi ya dawa wanazozihitaji kabla ya Mei 30.

"Maghala yatafungwa ili kuhesabu mali kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa fedha na yatafunguliwa Julai Mosi huduma zitakaporejea kama kawaida," inasomeka sehemu ya tangazo lililotolewa na MSD jana.

MSD inafanya hivyo kutekeleza sheria ya usimamizi wa fedha, inayotaka ukaguzi wa mali kabla mwaka husika wa fedha haujaisha.

Ujenzi machinjio Vingunguti kukamilika Julai

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wafanyabiashara wa machinjio ya Vingunguti wataendelea kusubiri mpaka Julai ujenzi utakapokamilika ili waanze kuitumia miundombinu hiyo iliyoboreshwa.

Hilo limebainishwa jana na naibu waziri wa mifugo na uvuvi, Abdallah Ulega aliyesema ujenzi huo wenye thamani ya Sh12.47 bilioni umekamilika kwa asilimia 85.

Kwa sasa alisema mradi upo katika hatua ya umaliziaji na ukikikamilika utakuwa na fursa nyingi za kiuchumi hivyo kuwataka wafanyabiashara kujitokeza kuwekeza katika sekta ya mifugo.

"Mashine zote zipo tayari, tuna uhakika hadi mwishoni mwa Julai tutakuwa tumekamilisha kila kitu. Harakisheni ujenzi kama viongozi wakuu walivyoagiza," alisema.

Ujenzi utakapokamilika, ngo'mbe 1,500 na mbuzi 1,000 watakuwa wakichinjwa katika machinjio hayo kwa siku na kutakuwa na kila aina ya ukataji unaohitajika na mteja.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara katika machinjio ya Vingunguti, Joel Meshack alimuahidi Ulega kutopandisha bei ya nyama kipindi hiki cha Sikukuu ya Eid.

12.47

Bilioni zinazotumika kukamilisha maboresho ya machinjio ya Vingunguti.

1,500

Ng'ombe wanaoweza kuchinjwa kila siku mradi ukikamilika.

"Wakati wa sikukuu uhitaji wa nyama huwa mkubwa sana. Tukileta ng'ombe 600 au 700 kwa mfano hawatoshelezi kabisa, ukienda mikoani nako wanapandisha bei ndio maana bei zinatofautiana na siku za kawaida," alisema Meshack.

Kwa upande wake, meya wa Ilala, Omar Kumbilamoto alisema manispaa imetenga eneo maalumu ambako wafanyabiashara wa mifugo watakuwa wakifanyia shughuli zao baada ya machinjio hayo ya kisasa kukamilika. Amesema eneo hilo limegharimu Sh500 milioni.

Ujenzi wa machinjio hayo unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ulianza Julai mwaka jana. Wakati wanakabidhiwa mradi huo, mhandisi wa shirika hilo, Elisante Ulomi alisema utachukua miezi 18 kukamilika.

Scanned with CamScanner

wiki, ikiwa ni sehemu ya msaada wa matangi manane kwa hospitali nne zilizochaguliwa za jiji hilo, kwa ajili ya kunawia mikono, ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona. Katikati ni Mfamasia wa hospitali hiyo, Simon Mbise. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Maadhimisho siku ya punda yalivyogeuzwa elimu corona

Na Jumbe Ismailly, SINGIDA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Singida kwa kushirikiana na shirika lisilokuwa la kiserikali la INADES Tanzania, wameadhimisha Siku ya Punda Duniani kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu tahadhari juu ya kujikinga na maambukizo ya corona.

Mtaalamu kutoka Idara ya Afya katika halmashauri hiyo, Neema Swai, alisema wadau hao walisaidia pia kutoa elimu kwa wananchi wa halmashauri hiyo juu ya umuhimu wa ufugaji wa punda na matumizi sahihi ya barakoa.

Alisema kwamba jamii kwa ujumla halmashauri imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji, lakini kwa kumtumia punda, wameweza kupata maji tiririka yanayosisitizwa na wataalamu hao kunawa ili kujikinga na ugonjwa huo.

"Mojawapo kati ya mbinu zinazotusaidia katika kukabiliana na hili janga, ni kunawa na majisafi yanayotiririka pamoja na sabuni. Kwa hiyo huyu mnyama punda tunaona katika jamii anasaidia kuchota maji... kwa hiyo jamii inakuwa na uhakika wa kupata maji na wanazingatia umuhimu wa kunawa majisafi tiririka pamoja na sabuni," alisisitiza Neema.

Neema alizitaja shughuli zingine zinazofanywa na punda ni humwingizia kipato mwananchi na kumwezesha kununua sabuni na kumwezesha kusimama katika misingi ya kukabiliana na janga la corona.

Alisisitiza kwamba mwananchi anapopata kipato kizuri kinachotokana na msaada wa mnyama punda, kunakuwa na uwezekano wa kupata lishe au mlo kamili ambao unamwezesha kuwa na kinga nzuri ya ugonjwa huo wa corona.

Ofisa Maendeleo ya Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Adamu Sungita, alisema punda amekuwa msaada mkubwa kwenye maeneo ya vijijini kwani huchota maji ya matumizi ya kawaida na maji ya kuendelea kutakasa mikono kwa ajili ya kujikinga na corona.

Kwa mujibu wa Sungita Halmashauri ya Wilaya ya Singida ina jumla ya punda 7,793, idadi ambayo ni ndogo kufananisha na idadi ya wanyama wengine wanaofungwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Sungita alisema wataendelea kutoa elimu kwa vijiji vingine vilivyobaki ili punda waendelee kutunzwa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Endesh, Kata ya Msange, Joseph Kingu, alifafanua kuwa tangu shirika lisilokuwa la kiserikali lilipoanza kufanya shughuli za mradi wa punda katika kijiji hicho, wameona manufaa yake.

Scanned with CamScanner

Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakinunua mbuzi katika mnada wa Vingunguti, jana, ambapo bei ya kitoweo hicho, ilionekana kupanda kuelekea sikukuu ya Eid El Fitr kutoka Sh. 80,000 mpaka 100,000 za awali, kwa mbuzi mmoja hadi kuanzia Sh. 100,000 mpaka 140,000. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Scanned with CamScanner